**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA**

Tarehe: 02/08/2023

# TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mafia anayo furaha kutangaza nafasi tano (**5**) za Ajira ya Kudumu kwa Watanzania wote wenye sifa stahiki ikiwemo **Mtendaji wa Kijiji III Nafasi 2, Mwandishi Mwendesha Ofisi II nafasi 2,** na **Msaidizi wa Kumbukumbu II nafasi 1.** Nafasi za ajira hizi zinatokana na Kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua **Kumb. Na. FA.170/375/01'B'/149** ya tarehe **10 Julai, 2023.**

## 1. MTENDAJI WA KIJIJI III NAFASI – (2)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mhitimu wa Kidato cha Nne/Sita mwenye Cheti/Astashahada (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo:-

- Utawala
- Maendeleo ya Jamii
- Usimamizi wa Fedha
- Sayansi ya Sanaa na Sheria

**MSHAHARA:**

Mshahara unaanza na ngazi ya TGS B

### 1.2 MAJUKUMU YA KUFANYA

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
2. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
4. Kuratibu mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
5. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji

6. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
7. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
9. Mwenyekiti wa Kikao cha wataalamu waliopo katika Kijiji
10. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
11. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji
12. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

## 2. MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II – (NAFASI 2)

### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na cheti cha Kidato cha Nne/Sita
- Awe na Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili
- Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza kwa maneno 80 kwa dakika moja na kupata mafunzo ya Programu za kompyuta za ofisi kama vile Word, Excel, Powerpoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**NGAZI YA MSHAHARA**
Mshahara unaanza na ngazi ya TGS C

### 2.2 KAZI NA MAJUKUMU

(i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida;
(ii) Kupokea wageni na kuwasaidi shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa;
(iii) Kutunza taarifa na kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine;
(iv) Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi
(v) Kupokea majalada na kusambaza kwa Maafisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika; na
(vi) Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika
(vii) Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali; na
(viii) Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi

## 3. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – (Nafasi 1)

### 3.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na cheti cha Kidato cha Nne/Sita
- Awe na Stashahada (Diploma) ya utunzaji kumbukumbu (NTA level 6) katika fani mojawapo ya masjala au Afya kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali
- Awe na ujuzi wa kompyuta

**NGAZI YA MSHAHARA**
Mshahara unaanza na ngazi ya TGS C

### 3.2 KAZI NA MAJUKUMU

- Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye rejista
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi
- Kusambaza majalada kwa watendaji
- Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa watendaji
- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji
- Kurudisha majalada kwenye shubaku/kabati la majalada au mahali pengine yanapohifadhiwa
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi

## 4. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE WA KAZI

a) Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa

b) Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA kama hana kitambulisho.

c) Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) yanayojitosheleza (detailed CV), Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45

d) Mwombaji lazima awe na anuani, namba za simu pamoja na majina na anuani za wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika

e) Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya kuhitimu mafunzo

f) Mwombaji aambatanishe picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni zenye rangi kwa muono wa nyuma (Background)

g) Testimonials, Provisional results, statement of results, hati za matokeo ya Kidato cha Nne au sita **HAZITAPOKELEWA**

h) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika (NACTE, NECTA, TCU, n.k)

i) Waombaji waliostaafishwa/kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba.

j) Uwasilishaji wa sifa na vyeti vya kughushi na ikabainika wahusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria

k) Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza

l) Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatafikiriwa.

m) Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 17/08/2023 SAA 9.30 ALASIRI**

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mafia,
13 Barabara ya Boma,
S.L.P. 85,
**61782 MAFIA.**

**Limetolewa na;**

....................................

MOHAMED H. OTHMAN

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**MAFIA**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MAFIA DISTRICT COUNCIL
03 AUG 2023
P. O. Box 85
MAFIA

**Nakala:**

Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira. www.ajira.go.tz
Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mafia. www.mafiadc.go.tz
Mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Mafia